

IDARA YA FEDHA NA BIASHARA

UTANGULIZI

Idara ya Fedha na Biashara ni moja kati ya idara zinazounda idara na vitengo 19 katika **Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama**. Idara ya Fedha na Biashara inafanya kazi zake katika maeneo makubwa 5; Fedha – Utawala, Fedha - Ufungaji wa Hesabu, Fedha - Matumizi, Fedha - Mapato na Fedha - Biashara na Masoko.

WATUMISHI IDARA YA FEDHA NA BIASHARA

Idadi ya watumishi waliopo katika Idara ya Fedha na Biashara ni 14 kati yao Mhasibu Mwandamizi – 01; Mhasibu Drj I – 01; Wahasibu Drj II – 03; Afisa Biashara Drj I – 01; Afisa Biashara Drj II – 01; Wasaidizi wa Mhasibu – 00; Wahasibu wasaidizi – 05; Mhudumu – 01; Katibu Mhtasi - 01

Jedwali Na 1: Hali ya Ikama Idara ya Fedha na Biashara.

S/N	Cheo cha Muundo	Mahitaji	Waliopo	Upungufu
1	Mhasibu Mkuu	1	0	1
2	Mhasibu Mwandamizi	2	1	1
3	Mhasibu Drj I	4	1	3
4	Mhasibu Drj II	4	3	1
5	Afisa Biashara I	1	1	0
6	Afisa Biashara II	2	1	1
7	Mhasibu Msaidizi	5	5	0
8	Msaidizi wa Mhasibu	2	0	2
9	Mhudumu	1	1	0
10	Katibu Muhtasi	1	1	0
	JUMLA	23	14	9

Chanzo: Ikama ya Watumishi ya mwaka 2017/2018

UTEKELEZAJI WA MPANGO KAZI NA VIPAUMBELE VYA IDARA.

Idara ya Fedha na Biashara katika kutekeleza Mpango Kazi na Vipaumbele vyake imekuwa ikizingatia Mpango Mkakati (Strateic Plan) wa Halmashauri ambao umetokana na Dira ya Taifa ya mwaka 2025, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka 5, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), Ilani ya Uchaguzi ya chama Tawala, Hotuba ya Mh Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa Bungeni tarehe 20 Novemba 2015 na Sheria mbalimbali zinazoongoza nchi yetu.

Katika kuzingatia maswala yaliyotajwa hapo juu mambo yafuatayo yamepewa kipaumbele na Idara ya Fedha na Biashara;-

1. Kusimamia Ukusanyaji wa Mapato ya Halmashauri kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa.
2. Kusimamia Matumizi ya Fedha za Umma kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Fedha za Umma.
3. Kusimamia Utoaji wa Taarifa za Fedha kila mwezi, robo mwaka na mwisho wa mwaka kulingana na Sheria, Kanuni na Taratibu, na kuziwasilisha kwenye mamlaka husika na Umma wa wananchi wa Mkalama.

Idara ya fedha siku zote imekuwa ikiongozwa na Sheria, Kanuni na Taratibu zifuatazo katika kutekeleza majukumu yake;

- a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (na marekebisho yake)
- b) Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sheria Na 9 ya 1982 na marekebisho yake
- c) Sheria ya Bajeti, Sheria Na 11 ya mwaka 2015 na Kanuni zake
- d) Sheria ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma, Sheria Na 7 ya mwaka 2011 na Kanuni zake
- e) Sheria ya Leseni za Biashara, Sheria Na 25 ya mwaka 1972 na Marekebisho yake na Sheria ya Vileo, Sheria Na 28 ya Mwaka 1968 na Marekebisho yake
- f) Kanuni za Usimamizi wa Fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (LAFM, 2009)
- g) Kanuni za Kudumu za Uendeshaji wa Halmashauri
- h) Kanuni za Uanzishwaji na Uendeshwaji wa Bodi za Zabuni katika mamlaka za Serikali za Mitaa za mwaka 2007
- i) Mwongozo wa Uhasibu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (LAAM,2009)
- j) Mwongozo wa Ukaguzi wa Ndani wa Mwaka 2005
- k) Mwongozo wa Mpango na Bajeti unaotolewa kila mwaka
- l) Miongozo mbalimbali inayoelekeza matumizi sahihi ya Mifumo inayotolewa na OR-TAMISEMI
- m) Sheria ndogo ya Halmashauri iliyozingatia Sheria mbalimbali za nchi na marekebisho yake
- n) Nyaraka (Circulars) mbalimbali zinazotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango

Imeandaliwa na,

CPA Piniel Philip
MWEKA HAZINA (W)
MKALAMA